**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule:0753640801**

**Makamu Mkuu wa Shule:0757017811**

**Mtaaluma mwandamizi:0747969930**

**Shule ya Sekondari:Kasoma**

**S.L.P:1382, Musoma**

**Tarehe:13/05/2026**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ..................................................**
**S.L.P ...............................**

Yah**: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KASOMA HALMASHAURI YA MUSOMA MKOA MARA MWAKA ...........</u>**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ............... na atasoma tahasusi ya HGK/HGL/HKL/HGLi/HGFa.

Shule ya Sekondari Kasoma ipo umbali wa Kilometa 50 Kusini mwa Mji wa Musoma na Kilometa 55 Magharibi mwa mji wa Bunda. Usafiri wa basi kutoka mjini Musoma unapatikana katika kituo cha Mabasi cha zamani nauli ni shilingi 5,000 kwa mabasi ya kwenda Majita kupitia barabara ya Majita road, Mugango, Kusenyi, Nyambui. Teremkia kituo cha Kasoma kibaoni, nauli ni shilingi 2,000 kwa pikipiki hadi shuleni.

Usafiri wa basi kutoka Bunda mjini unapatikana katika kituo cha mabasi cha Stendi mpya Bunda nauli shilingi 6,000 kwa mabasi ya kwenda majita kupitia barabara ya hospitali ya Manyamanyama, Saragana, Kusenyi, Nyambui. Teremkia kituo cha Kasoma kibaoni, nauli ni shilingi 2,000 kwa pikipiki hadi shuleni.

Muhula wa masomo unaanza tarehe ................ hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ................. saa 02:00 asubuhi siku ya Jumatatu, Ofisi ya Makamu wa mkuu wa shule itakuwa wazi kwa mapokezi na usajili ukiwa na vifaa kama ulivyoagizwa kwenye form hii.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1. Sare za Shule**

**i.** Sare ya shule hii ni sketi mbili za dark bluu zinazovuka magoti zikiwa na mshono wa rinda box na mfuko mmoja kwa Wasichana na suruali mbili za dark bluu zenye marinda mawili na mifuko mitatu zisizobana mwili ukubwa wa turn up inch 15 kwa Wavulana.

ii. Mashati mawili meupe yenye mikono mirefu.

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

iv. Sare ya Michezo ni track suit nyekundu pea moja (yenye mistari mitatu mieupe mikononi) na bukta nyekundu moja kwa wasichana na track suit pea moja ya bluu (yenye mistari mitatu mieupe mikononi) na bukta ya bluu kwa wavulana na raba nyeupe kwa wote.

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.

vi. Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana.

vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.

viii. Sweta rangi ya dark bluu yenye V shingoni.

ix. T-shirt mbili za rangi ya dark bluu nzito zenye color (zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh. 12,000/= kwa kila moja) kwa wavulana na wasichana,

x. Suruali mbili za rangi ya kijivu kwa wavulana na gauni mbili za kijivu mshono wa solo kwa wasichana.

xi. Tai mbili za rangi ya dark bluu.Tisheti moja yenye color ya mviringo ya rangi nyekundu kwa wasichana na rangi ya bluu kwa wavulana (inapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh. 8,000/=)

**2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari ya kaunta zisizopungua kumi(10);

ii. **Ream (A4)** ya karatasi aina ya **double A** Mbili (2) kwa mwaka, moja kila muhula;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika angalau kitabu kimoja kwa kila somo. **Advanced dictionary** kwa wanafunzi wanaosoma kingereza na **Kamusi** kwa wanaosoma kiswahili ni **LAZIMA** ;
iv. Scientific Calculator kwa michepuo ya HGK, HGL, HGLi na HGFa;
v. Godoro moja inchi mbili na nusu kwa sita( 2 ½ x 6);
vi. Mashuka ya bluu na pinki Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1, mto 1;
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
x. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mfagio 1 (soft broom), mfagio 1 mgumu (hard broom) Mfagio 1 wa nje (chelewa), Squeezer 1, kamba ya kuanikia nguo 1 .
xi. dawa ya chooni lita 5. (Inapatikana shuleni 12000/=)

**2.3. Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha zote zilipwe kwenye akaunti ya shule bank ya **NMB** akaunti numba **30301200331** jina **KASOMA SECONDARY SCHOOL.**

## Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

DAUD C MARWA
(MKUU WA SHULE)

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KASOMA
MUSOMA

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu**

**wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0753640801**
- **Makamu Mkuu wa Shule:0757017811**
- **Mwandamizi Taaluma:0747969930**
- **Mwandamizi Malezi na nidhamu:0687354776**

## ORODHA YA VITABU VYA KUNUNUA

Kila mwanafunzi anatakiwa kununua angalau kitabu kimoja kwa kila somo kwa kila tahasusi.

### HISTORY

1. Essentials in Advanced level History Paper 2 Based in new (2010) Syllabus, Written by Saleh Yasin.
2. Contemporary History Events Volume l. Writen by Shibitali CK. Tumain, Shibitali and Son Publisher.

### GEOGRAPHY

1. Practical Geography by Pritchard.
2. Geography an Integrated Approach, by David Waugh.
3. Principles of Physical Geography by Monkhouse.
4. Physical Geography in Diagrams by Bannet.
5. A Comprehensive Approach to Physical Geography for Secondary School (2019) by D T Msabila.
6. Human and Economic Geography Advanced Level paper 2 by DT Msabila.

**ENGLISH**

1. Advanced Level English: A Practical Approach (Second Edition) by Nicholous Asheli. (Paper one)
2. Advanced Level English: A Practical Approach (Second Edition) by Nicholous Asheli. (Paper two)
3. Oxford Advanced Learner's Dictionary.
4. Comprehensive Linguistics: English language 1 form 5&6.
5. Contemporary English for Advanced Level.
6. Advanced Learner’s English 1 by Shadrack Ndambo.
7. Advanced English Language by James John (Oxford).

**KISWAHILI**

1. Nadharia ya Fasihi Kidato cha 5 & 6 by J.A Masebo (2010).
2. Nadharia ya Kiswahili (kiswahili 1) Kidato cha 5 & 6 by J.A Masebo (2010).
3. Jikumbushe Kiswahili 2 Kidato cha 5&6 Maswali na majibu by Eliupendo W. Mbise na Leonard Mbikilwa.
4. Morani by Emmanuel Mbogo, Mfadhili by Hussein Tuwa, Vuta n’Kuvute by Shafi A Shafi, Kivuli Kinaishi by Said Mohamed, Kwenye Ukingo wa Thim by Ebrahim Hussein, Usiku Utakapokwisha by Mbunda Msokile, Kimbunga by Haji Gora, Chungu Tamu by Theobald A. Mvungi.
5. Kamusi.

**GENERAL STUDY**

1. Understanding General Studies Advanced Level Secondary School Education by Bigirwamungi

   J and Deogratius.

**SHULE YA SEKONDARI KASOMA**

**FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

i. JINAKAMILILAMWANAFUNZI:____________________________________________

ii. TAREHEYAKUZALIWA:________________KABILA_______________DINI_______________

iii. SHULE ALIYOTOKA:________________________________________

iv. MWANAFUNZI ANATOKA MTAA WA/KIJIJI CHA_________________________

v. KATA YA:____________________TARAFA YA________________________

vi. WILAYA YA_____________________MKOA WA:_____________________

vii. WAZAZI WOTE WAPO HAI/MMOJA YU-HAI/YATIMA (FUTA ISIYOHUSIKA)

viii. JINA KAMILI LA MZAZI/MLEZI_____________________________________

ix. KAZI YA MZAZI/MLEZI_____________________KAMA MLEZI TAJA UHUSIANO____________

x. ANUANI YA MZAZI/MLEZI________________________SIMU___________

1. Nimekubali nafasi niliyopewa na kuwa nitafuata sheria, kanuni na taratibu zote za shule. Sheria zote na kanuni za shule nimezisoma na kuzielewa.

2. Nitahakikisha na ninaahidi kuhudhuria darasani siku zote za masomo.

3. Nitahakikisha nasoma kwa bidii na maarifa. Sitashiriki katika vurugu za aina yoyote ile pindi nikiwa mwanafunzi hapa Kasoma sekondari. Naahidi nitadumisha nidhamu nzuri hapa shuleni.

4. Sitakuwa tayari kudhalilisha shule yangu.

5. Nitakubali kuchukuliwa hatua stahiki endapo nitakapoenda kinyume na sheria za shule.

**JINA LA MWANAFUNZI………………………………………………… TAREHE………………………………**

## FOMU YA AHADI YA MZAZI WA MWANAFUNZI

JINA LAMZAZI/MLEZI_____________________________________________

i. Nimesoma na kuyaelewa maelekezo na sheria za shule ya sekondari Kasoma aliyopewa mwanangu na ninakubaliana nayo.

ii. Ninakubali nafasi aliyopewa mwanangu.

iii. Nitahakikisha kuwa mwanangu anapata mahitaji yake yote muhimu ya shule.

iv. Nitakuwa bega kwa bega na walimu katika kuhakikisha kuwa mwanangu anafuata sheria na kanuni zilizo shuleni. Ni dhamu nzuri ya mtoto ndiyo mafanikio yake.

v. Naahidi kuwa mwanangu hatashiriki mgomo,fujo na wala makosa ya jinai kama yeye mwenyewe alivyoahidi. Ikitokea akikiuka hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.

vi. Tafadhali jaza majina, namba za simu na kuonyesha uhusiano uliopo kati ya ndugu/jamaa na mwanafunzi watakaokuja shuleni kumtembelea au kuwasiliana nae kwanjia ya simu kupitia uongozi wa shule.

| S / N | JINA | UHUSIANO | NA. SIMU | ANAKOISHI | KAZI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

-------------------------------- --------------------------------

**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI** **TAREHE**

NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI …………………………………………..

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

KASOMA SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 1382,
**MUSOMA.**

13/05/2026

The Medical Officer,
…………………………….

RE: ………………………………………………………………(Full name of student).

Please kindly examine the above named as to his/her Physical and mental for enrolment as a student, the examination should include the following categories.

1. (a)Eye–Sight (b) Hearing (c) Limbs (d) Speech (e) Venereal diseases (f) Leprosy (g) Epilepsy.
2. Neurosis.
3. Pregnancy.
4. Other serious diseases.

DAUD C MARWA
(MKUU WA SHULE)

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KASOMA
MUSOMA

**PART B MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a government Medical Officer)

I have examined the above named person and consider that he/she is physically FIT/UNFIT and mentally FIT/UNIFIT for fulltime of schooling.

1. (a)Eye–Sight…………………………………………………………

(b)Hearing……………………………………………………………………………

(c)Limbs……………………………………………………………………………….

(d)Speech……………………………………………………………………………

(e)Venereal diseases……………………………………………………………….

(f)Leprosy……………………………………………………………………………

(g)Epilepsy……………………………………………………………………………

2. Neuroses…………………………………………………………………

3.Pregnancy……………………………………………………………………………

4.Other serious diseases……………………………………………………………….

Date …………… Signature ……………………… Station ……………………… Designati........................................